JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Iddi Simba, (Mb.), Akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2000/2001

Viongozi mbalimbali hutembelea maonyesho ya Kimataifa ya DSM. Hapa Hayati Baba wa Taifa akitembelea moja ya mabanda.

KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI, DAR ES SALAAM — TANZANIA



Moja ya Zana za Kilimo katika Maonyesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam.



Maonyesho ya nguo zinazozalishwa katika viwanda vidogo-kwenye Maonyesho ya Kimataifa ya DSM.

HOTUBA YA WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA, MHESHIMIWA IDDI SIMBA, (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2000/2001

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha makusudio na shabaha ya makadirio ya matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2000/2001.

A. UTANGULIZI

2. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuelezea kwa undani hoja ya Wizara yangu, ningependa kwanza kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu walionitangulia kwa hotuba zao ambazo zimetoa ufafanuzi mzuri kuhusu mwelekeo na hali ya uchumi wetu. Aidha, mchango wenu Waheshimiwa Wabunge katika hoja zilizotangulia umesaidia serikali kufafanua mambo mbalimbali kuhusu maendeleo ya nchi yetu kiuchumi na kijamii, ikijumuisha sekta ya Viwanda na Biashara.

3. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 1999/2000 yamekuwepo matukio kadhaa ya majonzi makubwa kwa Taifa. Bunge lako Tukufu litakumbuka kuwa tumempoteza Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye alifariki dunia tarehe 14 Oktoba 1999. Baba wa Taifa ametufanyia mengi ambayo yanatufanya Watanzania tuheshimike popote duniani. Kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya Wizara, natoa rambirambi kwako wewe Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu na familia ya marehemu. Mwenyezi Mungu aiweke Roho ya Baba wa Taifa mahali pema peponi, Amin.

4. **Mheshimiwa Spika**, pia wabunge wenzetu ambao tulikuwa nao mwaka jana wakati kama huu hawapo nasi tena. Kwa niaba yangu na Wizara natoa rambirambi kwa familia, ndugu na jamaa wa Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliofariki dunia: Mheshimiwa Stanley M.J. Kinulo, Mbunge wa jimbo la Nyang'hwale; Mheshimiwa Salum Ngajulage, Mbunge wa jimbo la Liwale; na Mheshimiwa Col. Yusuf B. Ramia, Mbunge wa jimbo la Bagamoyo. Tunaomba Mola aziweke Roho za Marehemu mahala pema peponi, Amin.

5. **Mheshimiwa Spika**, naomba sasa nitumie nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioshinda katika chaguzi ndogo katika mwaka uliopita kama ifuatavyo: Mheshimiwa Dr. Ibrahim

Msabaha, Mbunge wa jimbo la Kibaha; Mheshimiwa Azim Suleiman Premji, Mbunge wa jimbo la Kigoma mjini; Mheshimiwa John Kibaso, Mbunge wa jimbo la Temeke; Mheshimiwa Phillipo Musalika, Mbunge wa jimbo la Nyang'hwale; na Mheshimiwa Sebastian Rukiza Kinyondo, Mbunge wa jimbo la Bukoba Vijijini. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge hao kwa ushindi uliowawezesha kujiunga nasi katika Bunge lako Tukufu.

B. UTEKELEZAJI WA MALENGO YA KIPINDI CHA 1999/2000

6. **Mheshimiwa Spika,** sasa napenda kuelezea kwa muhtasari utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea kwa kipindi cha 1999/2000.

Sekta ya Viwanda

Utendaji wa sekta

7. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 1999 sekta ya viwanda ilikua kwa asilimia 3.6 ikilinganishwa na asilimia 8.1 mwaka 1998. Aidha mchango wa sekta ya viwanda katika pato la Taifa ulikuwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na asilimia 8.3 katika kipindi hicho hicho. Ukuaji wa sekta ulipungua kutokana na

utashi mdogo wa soko la ndani la bidhaa za viwanda uliosababishwa na ushindani wa bidhaa kutoka nje na viwanda vingi vilivyobinafsishwa kuwa katika hatua za urekebishaji. Vile vile, ingawa upatikanaji wa umeme na maji ulikuwa wa kuridhisha ikilinganishwa na kipindi kilichopita, umeme wetu umekuwa wa gharama kubwa na hivyo kuchangia katika kuongeza gharama za uzalishaji na kupunguza matumizi ya uwezo uliopo. Sababu nyingine ya kushuka kwa ukuaji wa sekta ya viwanda ni uingizaji bidhaa kinyume na taratibu. Pamoja na hatua zilizochukuliwa na Serikali za kuzuia uingizaji wa bidhaa hafifu, yakiwemo matairi, bado kulikuwa na limbikizo (stock) kubwa kutoka nje ambayo imesababisha bidhaa za viwanda vyetu zilizolengwa na hatua hizi kuendelea kukosa soko.

Uzalishaji uliongezeka katika baadhi ya viwanda na hasa viwanda vilivyofanyiwa matengenezo makubwa na ambavyo vina masoko ya uhakika. Viwanda ambavyo uzalishaji umeongezeka ni pamoja na viwanda vya saruji, nguo, rangi, chibuku na mabati. Uzalishaji ulishuka katika viwanda vya bia, konyagi, chuma, betri, sigara, nyavu za uvuvi na kamba za katani.

Ajira katika Sekta ya Viwanda imeongezeka kutoka watu 137,000 mwaka 1998 hadi kufikia watu 145,000 mwaka 1999. Ongezeko hili

limetokana na uanzishaji wa viwanda vipya na ukarabati wa baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa. Pamoja na mafaniko haya, ajira katika baadhi ya viwanda vilivyobinafsishwa ilishuka kutokana na hatua za awali za urekebishaji mifumo, ukarabati wa mitambo na wakati mwingine wawekezaji kulazimika kupunguza ajira katika mashirika ambayo yaliajiri bila kuzingatia mahitaji halisi.

Wizara yangu inaendelea kuboresha mbinu mbalimbali za kulinda viwanda vyetu dhidi ya ushindani usio halali. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizi za Serikali, wenye viwanda hawana budi kuongeza juhudi za kutafuta masoko ya nje badala ya kutegemea soko la ndani tu. Hii ndiyo changamoto yangu kwa wanaviwanda wote.

Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo Ndogo.

8. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 1999/2000 sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo Ndogo imeendelea kutoa mchango mkubwa kwa Taifa katika maeneo ya ajira, uzalishaji, huduma na kuongeza pato kwa wananchi wa mijini na vijijini. Ili kuwasaidia wananchi hawa, Wizara inakamilisha sera mahususi kwa lengo la kuweka mazingira mazuri zaidi ya kukuza na kuendeleza viwanda na biashara ndogo ndogo. Aidha suala la mafunzo

limetiliwa umuhimu wa kipekee. Kwa mfano SIDO kwa kushirikiana na UNIDO ilitoa mafunzo ya usindikaji wa vyakula kwa wananchi 1500 katika kipindi cha mwaka 1999/2000, wengi wao wakiwa ni wanawake. Vile vile vikundi 25 vya Umoja wa Wana Viwanda na Biashara Ndogo Ndogo (VIBINDO) vilinufaika na mafunzo ya usindikaji wa vyakula pamoja na mafunzo ya uendeshaji wa biashara kwa kushirikisha taasisi za SIDO na TIRDO. Aidha, kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali, SIDO ilitoa mafunzo ya awali ya uanzishaji na uendelezaji wa viwanda na biashara ndogo kwa wananchi 1500.

9. **Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa wenye viwanda na biashara ndogo ndogo (National Enterpreneuship Development Fund – NEDF) tangu uanzishwe umeweza kusaidia uanzishaji wa miradi 8,256 yenye thamani ya Shs.2.6 bilioni na kutoa ajira kwa wananchi 12,051. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, mfuko uliweza kukidhi asilimia 15.2 tu ya maombi yapatayo 54,157 yenye thamani ya shs.21.5 bilioni. Kwa hiyo bado kuna haja ya kuendelea kutafuta vyanzo zaidi vya kutunisha mfuko huo ili kukidhi zaidi mahitaji ya wananchi ya kuanzisha viwanda na biashara ndogo ndogo.

Utekelezaji wa Sera ya Viwanda

10. **Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza Sera ya Viwanda, utafiti kuhusu mfumo wa mawasiliano kati ya Wanaviwanda na Serikali umekamilika. Hatua inayofuata sasa ni kupambanua njia sahihi ya utekelezaji wake. Aidha utafiti kuhusu matatizo ya sekta ya ngozi pia umekamilika na hatua za utekelezaji zitaanza kuandaliwa. Uchambuzi wa sekta ya viwanda (Industrial Survey) unaendelea. Aidha, katika uendelezaji teknolojia, akina mama 85 wamepatiwa mafunzo katika nyanja za ufumaji na uwekaji rangi kwenye nguo. Pia uandaaji wa Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo Ndogo unaendelea. Wakati huo huo, kama sehemu ya kutekeleza sera ya viwanda, suala la utoaji wa taarifa za msingi kuhusu sekta ya viwanda limepewa kipaumbele. Tunatarajia hivi karibuni, Wizara itatoa toleo la kwanza la jarida (bulletin) kuhusu sekta ya viwanda na biashara. Lengo ni kutoa jarida hili kila miezi sita na hatimae kila miezi mitatu.

Sekta ya Biashara

Utendaji

11. **Mheshimiwa Spika,** Sekta ya Biashara ilikua kwa asilimia 6 mwaka 1999 ikilinganishwa

na ukuaji wa asilimia 4.7 mwaka 1998. Aidha mchango wa sekta katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 15.9 mwaka 1998 hadi asilimia 16.1 mwaka 1999. Hali hii imetokana na kuimarishwa kwa miundombinu iliyoharibiwa na mvua za EL-NINO za mwaka 1997/98.

Biashara ya Ndani

12. **Mheshimiwa Spika,** usambazaji wa bidhaa nchini uliendelea kufanywa na wafanya biashara binafsi na makampuni machache ya umma. Hata hivyo bado kuna haja kubwa ya kupanua wigo wa waendeshaji wa biashara ya ndani. Bado sehemu kubwa ya biashara, hasa ya uagizaji, inashikiliwa na wafanyabiashara wachache sana. Hii ni aina fulani ya ukiritimba, hali ambayo haikubaliki. Ni suala la msingi kutafuta njia za kuongeza washiriki katika biashara hii. Pamoja na tatizo hili, Wizara imedumisha utaratibu wa kushirikiana na kushauriana na taasisi za wenye viwanda na wafanyabiashara kuboresha mazingira ya kibiashara. Katika misingi hii, Wizara imeongoza maandalizi ya uanzishaji wa Baraza la Taifa la Mashauriano (Tanzania National Business Council - TNBC).

Wizara yangu imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara mbalimbali kuhusu masharti ya kutakiwa kulipa kodi ya mapato kabla

ya kupewa leseni ya biashara. Wizara inafanya mashauriano na vyombo husika vya serikali ili kuona ni jinsi gani tunaweza kutenganisha masuala ya kodi na utoaji wa leseni za biashara bila kuathiri mapato ya Serikali. Aidha, Wizara yangu imeanza kuchukua hatua za kurejea (review) sheria za leseni ya biashara ya mwaka 1972 ili ikidhi matakwa ya sasa ya kibiashara.

Wizara imeendelea kutafiti uwezekano wa kuanzisha Bodi ya Biashara. Jambo la msingi kwa Wizara yangu ni kuona mtandao wa biashara ya kisasa unajengeka nchi nzima na unaendeshwa na Watanzania wenyewe. Hili ni eneo ambalo nina imani Watanzania wenyewe wanaliweza. Kuhusiana na eneo hili, napenda nitumie nafasi hii kulipongeza Shirikisho la Vyama vya Wanawake Tanzania (The Federation of Associations of Women Entrepreneurs in Tanzania - FAWETA) kwa kufungua matawi mengi mikoani. Naamini jitihada hizo zitasaidia kuunganisha wanawake wafanyabiashara nchini kote na hivyo kujenga msingi imara wa wafanyabiashara wazalendo.

Biashara ya Nje

13. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 1999 mauzo yetu nje yalikuwa ya thamani ya dola za Kimarekani 541 milioni ukilinganisha na mauzo ya

thamani ya dola za Kimarekani 588.5 milioni mwaka 1998. Manunuzi yetu ya bidhaa kutoka nje mwaka 1999 yaliongezeka na kufikia thamani ya dola za Kimarekani 1418.6 milioni ukilinganisha na manunuzi yetu ya mwaka 1998 ya dola za Kimarekani 1366 milioni. Mauzo nje mwaka 1999 yalilipia asilimia 38 tu ya manunuzi kutoka nje ikilinganishwa na asilimia 43 mwaka 1998. Hii ni changamoto kwetu sote ya kuwepo kwa ulazima wa kuimarisha mikakati ya kukuza mauzo yetu nje. Sera ya biashara inayoendelea kuandaliwa itazingatia suala hili pia.

Urekebishaji wa Mashirika ya Umma

14. **Mheshimiwa Spika,** zoezi la urekebishaji wa Mashirika ya umma katika sekta ya Viwanda na Biashara liliendelea vizuri. Kampuni zilizopata wawekezaji ni pamoja na Kampuni ya kuunganisha bodi za magari ya "Burns and Blane", Kampuni ya bidhaa za Ngozi ya Morogoro, IMCO na Tembo Resort and Tours zilizokuwa chini ya kampuni ya Saruji, Mbeya. Kampuni ya Imara Security Co. iliyokuwa pia chini ya Kampuni ya Saruji Mbeya pamoja na makampuni ya Biashara ya Mikoa ya Iringa, Dodoma, Mara na Lindi ilibidi zifilisiwe. Ingawaje tulitarajia kukamilisha ubinafsishaji wa kampuni za SPM na Printpak, zoezi hili halikukamilika kutokana na matatizo

mbalimbali. Jitihada zinaendelea kukamilisha ubinafsishaji wa kampuni hizi.

Kuhusu Mashirika Mama yaliyo chini ya Wizara ambayo ni Saruji, NCI, TKAI, TLAI, SMC, BIT na NASACO zoezi la kuhitimisha shughuli zake linakamilishwa. Kimsingi zoezi la kubinafsisha Makampuni chini ya Wizara yangu linakaribia kukamilika. Viwanda vikubwa ambavyo bado ubinafsishaji wake haujakamilika ni pamoja na Kiwanda cha Karatasi Mgololo, Kiwanda cha Majembe cha Mbeya, Kiwanda cha Chuma cha Tanga, Kiwanda cha kuunda mashine cha Kilimanjaro, Shirika la Vyuma la Taifa na Kiwanda cha Madawa ya Mimea cha Moshi. Inatarajiwa mengi ya mashirika haya yatabinafsishwa katika kipindi cha 2000/2001.

Suala la kufuatilia utendaji katika viwanda vilivyo binafsishwa ni muhimu. Hii inatuwezesha siyo tu kuhakiki kama wawekezaji wanatekeleza mahitaji ya mikataba ya mauzo ya hisa, bali pia kuelewa matatizo wanayokumbana nayo ili kwa pamoja tupate ufumbuzi wa matatizo hayo. Katika misingi hii, Wizara inaweka kipaumbele katika kuwasiliana na wawekezaji husika ili kujua matokeo ya zoezi la ubinafsishaji katika maeneo ya msingi kama vile uwekezaji halisi, uzalishaji, ajira, mauzo nje na mapato ya serikali.

Matokeo ya awali yanaonyesha mafanikio ya kuridhisha kwa baadhi ya viwanda. Mifano ni kiwanda cha bia cha Dar es Salaam (TBL), kiwanda cha sigara, kiwanda cha vifaa vya umeme cha Arusha, viwanda vya saruji vya Tanga, Mbeya na Dar es Salaam, kiwanda cha mablanketi cha Dar es Salaam n.k. Tumepata pia bahati ya kupata wawekezaji wakubwa wa kutoka nchi mbali mbali ambao waliitikia mwito wetu katika zoezi la ubinafsishaji. Mfano ni Kampuni ya ABB ya Norway, SCANCEM na SWEDFUND za Norway na Sweden, Holderbank na RJ Reylnolds za Uswisi, Dieqiu ya China, CDC ya Uingereza n.k. Ni matarajio yangu kwamba wawekezaji wakubwa wa aina hii wataendelea kujitokeza katika zoezi la ubinafsishaji wa makampuni ambayo hayajapata wawekezaji katika sekta ya Viwanda na Biashara.

Ushirikiano wa Kimataifa

Jumuiya ya nchi za Afrika Mashariki (EAC)

15. **Mheshimiwa Spika,** majadiliano kuhusu mkataba wa kuanzisha ushirikiano wa nchi za Afrika Mashariki yalikwishakamilika na mkataba ulitiwa saini mwezi Novemba 1999. Kuhusu sekta ya Viwanda na Biashara masuala yaliyokamilishwa ni pamoja na utafiti kuhusu mfumo wa biashara utakaotumika baina ya nchi

wanachama. Taarifa husika imekwisha pokelewa na nchi wanachama. Taarifa hii itatumika kama hadidu za rejea wakati wa kujadili uanzishaji wa mkataba wa biashara na ushirikiano wa forodha kwa nchi za Afrika Mashariki. Aidha mkakati wa kuendeleza viwanda kwa nchi za Afrika Mashariki nao umekamilishwa na taarifa yake imepelekwa kwa nchi wanachama kwa maoni. Taarifa hii ipo katika hatua ya kuhakikiwa.

Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC)

16. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu iliendelea kuratibu masuala ya Viwanda na Biashara katika nchi za SADC. Masuala hayo ni pamoja na kukamilisha sera ya maendeleo ya viwanda katika nchi za SADC na kufanikisha majadiliano juu ya uanzishaji wa soko la pamoja. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba kutokana na matarajio ya nchi wanachama ya kukuza uchumi kupitia ushirikiano wa kibiashara, Mkataba wa Biashara (Trade Protocal) umeridhiwa na zaidi ya theluthi mbili ya nchi wanachama na kwa hiyo mkataba umeanza kufanya kazi tangu tarehe 25 Januari, 2000. Nchi za Angola, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Seychelles bado zinasubiriwa kutia saini. Kutokana na maendeleo ya ushirikiano huu,

makubaliano katika kuendeleza huduma za viwango na ubora wa bidhaa yamesainiwa na nchi nyingi wanachama na yameanza kutekelezwa. Tunategemea kwamba juhudi za kuanzisha soko huru la nchi za SADC zitakamilika ifikapo tarehe 1 Septemba, 2000 ambapo soko hilo litazinduliwa rasmi. Maeneo ambayo yanaendelea kujadiliwa ni pamoja na kutafuta muafaka kuhusu viwango vya ushuru na ratiba ya upunguzaji viwango; vikwazo vya kibiashara visivyo vya kiushuru (non-tarrif barriers); masuala ya vigezo vya uasili wa bidhaa (rules of origin) na mfumo wa chombo cha kusimamia utekelezaji wa Mkataba wa Biashara. Lengo la nchi Wanachama ni kuafikiana katika sehemu kubwa ya maeneo haya kabla ya uzinduzi rasmi wa soko huru la SADC.

Shirika La Biashara Duniani (World Trade Organisation – WTO)

17. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu shughuli za WTO, Wizara yangu mnamo mwezi Mei, 2000 iliandaa kongamano na Semina ya kitaifa kwa ajili ya viongozi wa ngazi za juu kwa lengo la kuwaelimisha kuhusu mfumo wa biashara chini ya WTO, hususani kuhusu manufaa na athari zake kwa uchumi wetu. Aidha Wizara ilitekeleza wajibu wake wa kuandaa na kufanikisha mkutano wa mashauriano na nchi wafadhili na taasisi za Kimataifa chini ya utaratibu wa Integrated

Framework for Trade Development (IF), kama ilivyokubaliwa na Mawaziri wa Biashara Duniani walipokutana Singapore, kufanya marejeo ya mwenendo wa utekelezaji wa makubaliano ya Uruguay.

18. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa taarifa kuwa mkutano wa WTO wa Mawaziri wa Biashara Duniani uliofanyika Novemba, 1999 Seattle, Marekani haukufanikiwa. Hali hii ilitokana na nchi zinazoendelea kutokuwa tayari kuanzisha duru nyingine ya majadiliano wakati nchi changa hazijaweza kutekeleza yale yaliyokubaliwa mwaka 1994. Tanzania itaendelea kushirikiana na nchi nyingine zinazoendelea kuishinikiza WTO kutambua udhaifu wa uchumi wetu na hivyo kutoa unafuu unaokubalika.

Usimamiaji wa Sheria

Sheria ya Usajili wa Biashara na Leseni za Viwanda

19. **Mheshimiwa Spika**, zoezi la kubadili Kitengo cha Usajili, Sheria za Biashara na Leseni za Viwanda kuwa Wakala wa Serikali lilikamilika Desemba, 1999. Aidha taratibu za kuhamisha shughuli za utoaji wa leseni za biashara kutoka Idara ya Biashara kwenda katika Wakala zinaendelea. Wakala imekwishaanza kusimamia

utekelezaji wa sheria za Hatimiliki na Hakishiriki Na.7 ya mwaka 1999, iliyopitishwa April mwaka 1999 na kuanza kutumika tarehe 31/12/1999. Hivyo yeyote mwenye haki ambazo zinatumiwa bila ridhaa yake, ana haki ya kushtaki chini ya Sheria hiyo. Aidha kanuni mpya za Alama za Biashara na Huduma (Trade and Service Marks Regulations) za mwaka 2000, zilizotungwa chini ya sheria ya Alama za Biashara na Huduma Na.12 ya 1986 zimeanza kutumika. Wakala pia imeanza kutoa hataza chini ya sheria mpya ya hataza Na.1 ya 1987.

Mizani na Vipimo

20. **Mheshimiwa Spika,** Kitengo cha Mizani na Vipimo kiliongeza juhudi za kuielimisha jamii kuhusu umuhimu wa Sheria ya Mizani na Vipimo na matumizi yake. Kazi hiyo ilifanyika kupitia magazetini na vipindi maalum katika televisheni. Kazi ya msingi inayoendelea sasa ni kubadili Kitengo hiki kuwa Wakala.

Udhibiti wa Viwango

21. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na kuongezeka kwa majukumu ya Shirika la Viwango (TBS) katika mazingira ya soko huria, Shirika lilibuni na kuanza kutekeleza mkakati wa kudhibiti bidhaa duni kutoka nje ya nchi. Utekelezaji wa

mkakati huo unafanywa kwa ushirikiano wa karibu na Mamlaka ya Mapato (TRA). Kazi hiyo imeanzia katika bandari ya Dar es Salaam na baadaye itahusisha vituo vingine katika mipaka yetu.

Maadili ya Biashara

22. **Mheshimiwa Spika**, napenda kueleza kwamba Baraza la Maadili ya Biashara liliundwa mwezi Desemba 1999, kufuatia uteuzi wa Mwenyekiti na wajumbe wa Baraza. Aidha Msajili wa Baraza ambaye ni mtendaji mkuu wa Baraza hilo amekwishateuliwa. Baraza litafanya kazi zake kwa ushirikiano wa karibu na Kitengo cha Maadili ya Biashara. Vyombo hivi viwili vitasimamia sheria ya kulinda maadili ya ushindani katika uchumi, ili kuondoa ukiritimba, migongano kwenye soko pamoja na kulinda haki ya watumiaji wa bidhaa na huduma mbali mbali. Wizara pia inaendelea kukamilisha muundo wa Kitengo cha Maadili ya Biashara ili kuiwezesha serikali kuteua maafisa na wafanyakazi wengine wa Kitengo hiki.

Uimarishaji wa Taasisi za Viwanda na Biashara

Uendelezaji wa Viwanda

23. **Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana,

Serikali ilikwishafanya maamuzi ya kuwa NDC itaendelea kuwa Shirika la Umma la kuendeleza miradi ya viwanda vikubwa na kuwa mshauri wa Serikali katika eneo hili. Pamoja na majukumu haya, Serikali imeipa NDC mamlaka maalum katika kushughulikia miradi maalum. Miradi hiyo ni pamoja na miradi ya Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara (Mtwara Development Corridor) na Maeneo Maalum ya kuzalisha bidhaa kwa ajili ya masoko ya nje (Export Processing Zones). Aidha, NDC inaendelea na utekelezaji wa mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia makaa hayo. Shirika limechukua hatua za kutafuta ubia na makampuni ya nje kwa lengo la kutekeleza miradi ya kiuchumi hapa nchini.

24. **Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza majukumu yake mapya kwa ukamilifu, NDC imebuni mikakati na mbinu mbalimbali za kuweza kuongeza kipato chake. Mojawapo ni kufanya majengo yake kuwa ya kibiashara. Aidha Shirika limefanya jitihada za kupata fedha kutoka kwenye masoko ya fedha ya nchini na ya kimataifa kwa kutumia mali halisi za shirika kama kinga. Jitihada hizi zinaonyesha matumaini.

25. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada hizo, NDC bado inakabiliwa na matatizo ya kifedha, hasa ikizingatiwa ukubwa wa majukumu

iliyopewa. Hali hii inasababishwa na kukosekana kwa vyanzo vya uhakika vya mapato kwa Shirika, hasa baada ya kurejesha Serikalini hisa zote za mashirika yaliyokuwa chini yake. Aidha Sheria ya Mashirika ya Umma haitoi nafasi kwa NDC ya kushirikiana vizuri na wabia binafsi. Kutokana na hali hii Wizara yangu imeteua Kamati ya Serikali ya kuchambua masuala haya na kuyatolea mapendekezo. Kamati imekwisha anza kazi yake na tayari imekamilisha rasimu ya sheria ya kuunda Shirika hili upya na itakayowezesha NDC kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

26. **Mheshimiwa Spika, n**apenda kuliarifu Bunge lako kuwa mikakati na mbinu za kuimarisha SIDO inaandaliwa. Kwa kuanzia, utafiti ume-fanywa na wataalam wa SIDO kwa kushirikiana na GTZ na hivi sasa utafiti huo unafanyiwa uchambuzi na viongozi wa SIDO ili kutoa mapendekezo kwa Serikali kwa maamuzi. Aidha, SIDO iliendelea kutekeleza mabadiliko ya muundo wa Shirika ambapo madaraka zaidi yamepelekwa mikoani ili kuweza kuhudumia walengwa kwa karibu zaidi. Menejimenti za SIDO mikoani zimepewa majukumu na madaraka juu ya huduma watakazotoa kwa kushirikiana na Makao Makuu. Mkazo unatiliwa zaidi katika huduma chache muhimu zinazotakiwa zaidi na walengwa (demand driven) zikiwa ni pamoja na ushauri, mafunzo,

mikopo, masoko na utetezi. Ili kutekeleza kazi hii kwa ufanisi kila mkoa umeandaa na kutekeleza mipango ya kibiashara (Business Plan).

Ukuzaji Mauzo Nje

27. **Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Biashara ya Nje (BET) iliendelea na jukumu la kutafiti masoko ya bidhaa zetu. BET ilifanya utafiti wa masoko ya nje kwa bidhaa za nguo, katani, mbegu za mafuta, asali na nta. Katika jitihada hizi BET ilifanikiwa kupata soko la asali na nta katika nchi za Dubai, Ujerumani, Ubelgiji na Uholanzi. Kwa upande wa nguo, utafiti umeonyesha kuwa viwanda vya Urafiki, Blanketi, Ubungo Spinning, Afritex, Sunflag na A to Z Ltd. vinaweza kutengeneza bidhaa zinazoweza kuuzwa nje ya nchi.

28. **Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 1999/2000 Tanzania ilishiriki katika maonyesho ya biashara ya Kimataifa Maputo, Msumbiji; China; Fukuoka, Tokyo na Osaka, Japan; na Expo 2000 Hannover, Ujerumani. Aidha, maonyesho ya 23 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofanyika kati ya tarehe 1 hadi 9 Julai, 1999 yalionyesha mafanikio makubwa. Maonyesho hayo yalijumuisha vikundi vya akina mama 310 kutoka mikoa yote 25 ya Tanzania, ambavyo vilidhaminiwa na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF) na wanawake washiriki waliojitegemea.

Katika maonyesho hayo nchi 13 za nje zilishiriki na jumla ya nchi 32 ziliwakilishwa na makampuni binafsi.

Huduma za teknolojia na utafiti

29. **Mheshimiwa Spika,** licha ya NDC, SIDO, TBS na BET, Wizara yangu inazo taasisi za huduma za teknolojia ambazo ni muhimu katika kufanya utafiti kwa maendeleo ya Viwanda. Pamoja na umuhimu wake taasisi hizi bado zimeendelea kufanya kazi katika mazingira magumu kutokana na ufinyu wa bajeti. Taasisi zinazohusika ni pamoja na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (TIRDO), Kituo cha Kueneza Teknolojia rahisi vijijini (CAMARTEC) na Shirika la Ubunifu wa Mitambo (TEMDO). Taasisi zingine ni zile zinazoshughulikia uendelezaji wa ufundi stadi (HPTC), utoaji wa huduma za ushauri kwa viwanda na biashara (TISCO) na utoaji wa elimu ya biashara (CBE).

30. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na ufinyu wa Bajeti, Taasisi hizi ziliendelea kutekeleza majukumu yake japo kwa ufanisi mdogo. Kwa mfano katika mwaka 1999/2000, TIRDO wameendelea na utafiti wa malighafi inayotokana na bidhaa za masalia ya mazao (agro-waste) ambayo ni makapi ya kahawa, mpunga na makumbi ya nazi, zote zikiwa ni malighafi ya hapa

nchini. Mifano mingine ya utafiti uliofanywa na TIRDO ni gundi ya mbao, dawa inayotokana na utomvu wa korosho ya kuulia wadudu wanaoharibu mbao na bidhaa za mbao, usindikaji wa asili wa muhogo na utengenezaji wa chaki. Aidha Shirika limetoa mafunzo kwa ajili ya wafanyabiashara wenye viwanda vidogo vidogo (VIBINDO) kuhusu usindikaji wa vyakula. Shirika la TEMDO limeendeleza jukumu lake la kubuni mashine rahisi zinazoweza kutumika vijijini kama vile mashine za kukoboa na kusaga nafaka mbalimbali. Kituo cha CAMARTEC kimekuwa mstari wa mbele katika kubuni na kuendeleza nishati mbadala (alternative sources of energy) ikiwemo majiko ya kutumia biogas, mionzi ya jua na pumba za mpunga kwa ngazi ya familia, vyuo, mashule, kambi za askari na mahoteli. Kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), kituo kiliunda na kusambaza mashine za kukata malisho ya mifugo (forage choppers) ambazo zinawasaidia wafugaji wa kisasa wanaofuga mifugo ndani kwa ndani (zero grazing). Aidha wakulima wameanza kutumia vihenge vilivyobuniwa na CAMARTEC inavyo-hifadhi nafaka bila kutumia madawa, kitu ambacho kinaepusha athari za kemikali katika chakula.

31. **Mheshimiwa Spika,** Chuo cha High Precision Technology Centre (HPTC) kimekuwa kikitoa mafunzo chini ya mkataba na Chuo cha

VETA Chang'ombe, hatua ambayo imeongeza matumizi ya Chuo kufikia asilimia 90 ya malengo. Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kiliendelea kutoa mafunzo ya elimu ya biashara katika vituo vyake vya Dodoma na Dar es Salaam. Mafunzo yanayotolewa ni katika ngazi ya vyeti na stashahada kwa Wakaguzi wa Mizani na Vipimo, Biashara, Uhasibu na Ugavi. Katika kipindi cha 1999/2000, Chuo kiliandikisha wanafunzi 615 ambao waliweza kumudu kujilipia gharama ikizingatiwa kuwa Serikali imesitisha kulipia gharama za wanafunzi. Lengo la Wizara ni kukisaidia chuo kubuni mbinu za kujitegemea ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha waajiri na wazazi kugharamia mafunzo. Aidha itabidi Chuo kiwe na ushirikiano wa karibu na waajiri ili kubaini taaluma za kisasa za kibiashara zinazohitajika na waajiri.

Kuimarisha uwezo wa Wizara

32. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ufanisi wa kazi wizarani, Wizara yangu imefanikiwa kutoa mafunzo katika fani mbalimbali kwa baadhi ya wafanyakazi ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kompyuta, mambo ya sheria, utunzaji wa kumbukumbu, uhandisi, uchumi na utawala. Aidha, Wizara imeweka kipaumbele katika jukumu la kuendeleza Watumishi wake kwa njia ya mafunzo na vitendea kazi kwa kushirikiana na

taasisi mbalimbali ikiwa ni pamoja na JICA, UNIDO, WTO na Sekretarieti ya Jumuia ya Commonwealth.

Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali

33. **Mheshimiwa Spika,** kuhusu ukusanyaji wa mapato ya Serikali, katika mwaka 1999/2000, hadi Aprili, 2000 Wizara iliweza kukusanya jumla ya Sh. 605.5 milioni kupitia Wakala wa Usajili wa Makampuni na Leseni za Viwanda, na Kitengo cha Mizani na Vipimo. Aidha shughuli za utoaji wa leseni za biashara zililiingizia Taifa jumla ya Sh. 6.5 bilioni.

34. **Mheshimiwa Spika**, Wizara inaratajia katika mwaka 2000/2001 kukusanya jumla ya 1.02 bilioni kupitia Wakala wa Usajili wa Makampuni na Leseni za Viwanda na Kitengo cha Mizani na Vipimo. Aidha shilingi 6.8 bilioni zinatarajiwa kukusanywa kutokana na utoaji wa leseni za biashara.

c. MALENGO KWA MWAKA 2000/2001

35. **Mheshimiwa Spika,** katika kuelezea malengo ya Wizara kwa kipindi 2000/2001 ningependa kwanza kueleza kwa kifupi matatizo ya kutokua haraka kwa uchumi wetu. Kama sote tunavyofahamu, nchi yetu bado inakabiliwa na matatizo ya umasikini. Matatizo haya tumekuwa

tukijitahidi kuyatafutia ufumbuzi kwa kipindi chote cha uhuru wetu. Japo yapo mafanikio, bado mafanikio haya ni madogo. Hali hii imetokana kwa kiasi fulani na uchumi wetu kuwa tegemezi. Sekta kuu ya uchumi wa nchi yetu ambayo inaajiri asilimia kubwa ya wananchi na kuchangia asilimia zaidi ya hamsini ya Pato la Taifa ni kilimo. Kilimo chetu kwa sehemu kubwa ni cha jadi na ni cha kujikimu (subsistance). Ili sekta hii ijengeke haraka na kutuondoa katika umasikini, inabidi uwepo uhusiano wa karibu na sekta nyingine, hususani sekta za viwanda na elimu. Uhusiano huu utasaidia sana kuongeza tija katika sekta hii. Tija itaongezeka kutokana na matumizi ya teknolojia ya kisasa, uongezaji wa thamani ya mazao kutokana na usindikaji na matumizi ya elimu ya kisasa katika uzalishaji na uhifadhi wa mazao.

36. **Mheshimiwa Spika**, njia ya kuondokana na umasikini ni kutekeleza lengo kuu la mwelekeo mpya wa Sera za CCM la kujenga msingi wa uchumi wa kisasa wa Taifa linalojitegemea na uwezeshaji wa kiuchumi (economic empowerment) wa wananchi walio wengi. Lengo ni kuwa na uchumi unaoendeshwa kwa maarifa ya kisayansi na kiteknolojia. Tunatakiwa tuwe na uwezo wa kuzalisha bidhaa kwa wingi kwa ajili ya mahitaji ya ndani na kwa soko la nje ili tujenge

uwezo wetu wenyewe wa kununua mahitaji yetu kutoka nje kwa bidhaa ambazo hatuzalishi.

37. **Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha malengo haya, mkakati sahihi ni kuendeleza sekta za uzalishaji na hasa zile zinazochochea maendeleo ya sekta nyingine. Sekta ya viwanda ni mojawapo ya sekta hizo. Sekta hii ni chimbuko la uchumi wa kisasa. Sekta ya viwanda ina nguvu kubwa ya kuziingiza sekta nyingine za uchumi katika uchumi wa kisasa. Kwa hiyo, sekta ya viwanda inabidi ipewe uzito unaostahili. Kwa kutambua ukweli huu, Wizara yangu itaendelea na jukumu la ufufuaji wa viwanda vilivyopo nchini hasa vya nguo, ngozi, kanvasi, usindikaji wa mazao ya kilimo, mbao na madawa kwa kuwahamasisha wawekezaji. Aidha, kipaumbele kitatolewa kwenye suala la Utafiti na kuweka mtandao bora wa taasisi za utafiti nchini pamoja na kuziwezesha taasisi hizi kuyafikisha matokeo ya utafiti kwenye soko. Wizara pia itaendelea na juhudi za kufufua na kuimarisha viwanda na miundo mbinu ya utengenezaji wa vifaa na mitambo ya chuma kwa kushirikisha wawekezaji. Katika misingi hii tutendelea kutafuta wawekezaji katika miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga kwa lengo la kuipatia nchi yetu msingi wa viwanda mama.

38. **Mheshimiwa Spika,** kama nilivyotamka wakati nikiwasilisha Makadirio ya Wizara yangu mwaka jana, Wizara inatarajia kuyatumia zaidi mashirika ya SIDO na NDC kuwaendeleza Watanzania kiuchumi. Wizara itaendelea kulipa uwezo Shirika la SIDO ili liweze kueneza viwanda vidogo na biashara ndogo ndogo kwa ufanisi zaidi. Sera ya Viwanda Vidogo inayoandaliwa italenga kutimiza lengo hili. Shirika la NDC litahusika na kuwashirikisha wananchi katika kumiliki na kuendesha miradi ya kati na mikubwa ya viwanda. Sheria ya kuunda NDC inayofanyiwa marekebisho italenga katika kutimiza lengo hili. Aidha Wizara itaendelea kuwa na mawasiliano ya karibu na Jumuia za Wafanyabiashara na Wenye viwanda ili kujua matatizo yao na kuyapatia ufumbuzi kila inapowezekana.

39. **Mheshimiwa Spika,** kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu, Tanzania ni nchi mwanachama wa WTO. Aidha, Tanzania ni mwanachama wa SADC na EAC. Hii ina maana kuwa tunalazimika kujiandaa kikamilifu ili tunufaike katika masoko ya SADC na EAC na katika mfumo wa biashara wa WTO. Hivyo basi, kuna haja ya kuboresha sekta zote: kilimo, viwanda, maliasili, madini n.k. Kuna haja pia kubuni mbinu mpya za kibiashara ili tuweze kuhimili mashindano kama nchi katika masoko haya. Kwa hiyo tuna jukumu

kubwa la kuimarisha taasisi za uzalishaji, kukuza biashara na kudhibiti ubora wa bidhaa. Wizara yangu ina majukumu ya kuimarisha shirika la TBS linaloshughulikia viwango vya ubora wa bidhaa, kwa lengo la kuziwezesha kushindana hasa katika masoko ya nje. Tunalo jukumu pia la kuhakikisha maadili ya biashara yanazingatiwa katika ngazi za kisera na kisheria. Iwapo wafanyabiashara wetu hawatazingatia maadili ya biashara watajikuta wanakumbana na vikwazo katika masoko yote, ya ndani na ya nje.

40. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na maelezo haya ya jumla, malengo ya Wizara kwa kipindi cha 2000/2001 yatakayopewa kipaumbele ni pamoja na:-

a) Kuongeza uwezo wa Wizara kusimamia na kuendeleza shughuli za Viwanda na Biashara kwa kuwapa wafanyakazi mafunzo na vitendea kazi kulingana na mahitaji ya maeneo yao ya uwajibikaji.

b) Kuainisha mipango na programu za Wizara ili ziendane na Dira ya Taifa (Vision 2025)

c) Kuimarisha utendaji wa vyombo vya kuendeleza viwanda na biashara ili sekta iweze kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa. Kipaumbele kitawekwa

katika kuimarisha taasisi za Utafiti na Maendeleo (R&D), lengo likiwa kukuza utafiti wa kuviwezesha viwanda vyetu kutumia malighafi inayopatikana hapa nchini kila inapowezekana.

d) Kukuza na kuendeleza mahusiano ya Kimataifa katika eneo la viwanda na biashara kupitia vyombo vya ushirikiano hasa SADC, EAC na WTO.

e) Kukuza na kuendeleza sekta binafsi kwa kuanzisha mfumo mzuri wa mashauriano kati ya Serikali na sekta binafsi. Lengo ni kuanzisha Baraza la Taifa la Mashauriano (Tanzania National Business Council). Aidha kuziimarisha SIDO na NDC ili ziweze kutekeleza majukumu yao mapya ya kuimarisha na kuendeleza sekta binafsi.

f) Kuendelea na utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Viwanda kama sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Viwanda na Uandaaji wa Sera ya Viwanda vidogo na Biashara ndogo ndogo. Aidha programu hii italenga katika kuboresha mazingira ya uwekezaji, kuongeza ufanisi katika uzalishaji, kuendeleza teknolojia na ushindani na kulinda mazingira.

g) Kutekeleza programu za kuendeleza sekta ya biashara. Lengo kubwa la programu hii ni kukamilisha na kuanza utekelezaji wa Sera ya Biashara. Programu hii itahusisha pia utoaji wa mafunzo kwa Watanzania na hasa kwa wafanyabiashara na kwa taasisi za Serikali zinazohusika na biashara, ili kuongeza uelewa wao wa mfumo wa biashara chini ya WTO (Joint Integrated Technical Assistance Programme – JITAP). Vile vile programu hii itahusika na utekelezaji wa miradi ambayo itaiwezesha Tanzania kuwa na uwezo wa kushiriki vizuri katika mazingira ya biashara huria duniani (Integrated Framework – IF). Hii ni pamoja na miradi ya uhamasishaji wa mauzo nje, uanzishaji wa maeneo ya uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje (EPZ), uanzishaji wa mitaji kwa wauzaji bidhaa nje (Export Finance and Credit Guarantee Schemes) na uanzishaji wa Mfuko maalum wa ushindani na teknolojia ya ufungashaji bidhaa kwa ajili ya mauzo nje.

C. SHUKRANI

41. **Mheshimiwa Spika,** maandalizi ya Hotuba hii yamewezekana kutokana na ushirikiano mkubwa kati ya Uongozi na Watendaji ndani ya Wizara. Kwa hiyo napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Naibu Waziri, **Mhe. Shamim Khan (Mb),** Katibu Mkuu, **Prof. Joshua Doriye** na Maafisa na Watumishi wote wa Wizara na Mashirika ambao michango yao imesaidia sana katika kukamilisha Hotuba hii. Aidha nawashukuru sana Wafanyabiashara na Wanaviwanda mbalimbali ambao nimekuwa nikikutana nao mara kwa mara katika vikao maalum vya mawasiliano (interactive meetings). Michango yao katika vikao hivi imesaidia sana katika kutoa mwelekeo wa shughuli za Wizara unaozingatia matarajio ya washitiri (stakeholders) wakuu ambao ni wanaviwanda na wafanyabiashara. Vile vile nachukua nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika na wahisani mbali mbali kwa misaada yao iliyotuwezesha kusaidia kutekeleza miradi na programu mbalimbali katika sekta hii.

E. MAKADIRIO YA BAJETI YA MWAKA 2000/2001

Matumizi ya Maendeleo

42. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2000/2001, Wizara yangu inaomba kiasi cha Sh.379,000,000 kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo ikiwa zote ni fedha za nje kutoka kwa wafadhili ambao ni UNIDO, Sida na DANIDA. Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh.329,000,000 kitatumika kuendeleza utekelezaji wa Sera ya Viwanda, uandaaji wa Sera ya Viwanda Vidogo, uchambuzi wa matokeo ya Sera za kijumla kwa sekta ya Viwanda, uchambuzi na urejeaji (review) wa sheria zinazohusiana na sekta ya viwanda na biashara na uimarishaji wa Wizara (capacity building). Aidha, kiasi kilichobaki cha Sh.50,000,000 kitatumika katika uandaaji wa Sera ya Biashara. Ni matumaini yetu kwamba msaada huu utapatikana kutoka kwa Wafadhili kama ilivyokusudiwa.

Matumizi ya Kawaida

43. **Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza malengo ya sekta ya Viwanda na Biashara katika mwaka 2000/2001, Wizara yangu inaomba Sh.4,090,668,600 kwa matumizi ya Kawaida. Kati

ya fedha hizi, kiasi cha Sh. 1,338,581,260 ni matumizi ya Wizara yenyewe; Sh. 2,338,701,900 ni ruzuku kwa Mashirika ya Umma yanayosimamiwa na Wizara yangu na Sh. 413,385,440 ni kwa ajili ya matumizi ya Kitengo cha Mizani na Vipimo.

44. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na hotuba hii nimeambatisha majedwali mbalimbali ambayo yanatoa takwimu kama vielelezo zaidi vya hoja hii. Naamini vielelezo hivi vitawawezesha Waheshimiwa Wabunge kutafakari vizuri zaidi maendeleo katika sekta hii ya Viwanda na Biashara.

45. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

VIGEZO VYA UFANISI KATIKA SEKTA YA VIWAND
NA BIASHARA(Kwa bei za mwaka 1992)

Mwaka	Ajira katika Sekta ya Viwanda	Ukuaji halisi wa Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa	Mchango wa Sekta ya Viwanda kwa Pato la Taifa	Mchan Biasha Taifa
1988	111,537	3.1	8.7	
1989	119,822	5.2	9.0	
1990	122,937	4.1	8.8	
1991	121,374	1.9	8.7	
1992	125,655	-4.0	8.2	
1993	125,787	0.6	8.2	
1994	129,984	-0.2	8.1	
1995	130,554	1.6	7.9	
1996	129,248	4.8	8.0	
1997	131,832	5.0	8.1	
1998	137,014	8.1	8.4	
1999	144,537	3.6	8.3	
Wastani	127,523	2.82	6.7	

Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara

UZALISHAJI WA BAADHI YA BIDHAA VIWANDANI

Aina ya Bidhaa	Kipimo	1988	1989	1990	1991	1992	1993	1994	1995	19
Biskuti & tambi	Tani	1965	1315	1141	739	497	378	240	202	
Unga wa ngano	Tani	30190	21140	12140	2950	17010	7510	13930	11551	339
Konyagi	000 Lita	1172	1315	1203	1505	1879	1882	1966	2011	18
Bia	000 Lita	53000	53740	45040	49890	49390	57050	56845	89301	1250
Chibuku	000 Lita	15290	16260	13830	15460	13260	14770	10695	11319	140
Sigara	Millioni	2785	2846	3742	3870	3789	3893	3383	3699	37
Nguo	000 Mita	64330	67310	64110	54790	73410	60300	51350	31181	373
Kamba za katani	Tani	18490	18570	20920	21200	21800	25150	21312	17713	105
Nyavu za uvuvi	Tani	232	165	152	151	95	93	122	122	1
Tabaka za mbao	000 Tani	2250	1687	1525	1642	1162	673	486	283	3
Dawa za pareto	Tani	44	40	50	45	49	35	24	21	
Mbolea	Tani	5989	27030	17426	20620	-	-		-	-
Rangi	000 Lita	2079	2145	2184	2536	2354	2129	2016	3233	52
Bidhaa za petrol	000 Lita	438	411	337	337	357	348	340	398	3
Saruji	000 Tani	592	595	664	1023	677	749	686	739	7
chuma	Tani	9940	14900	9000	7560	6100	7110	7003	2518	77
Bati	Tani	14710	20240	21720	23400	24160	25860	22961	18142	64
Aluminium	Tani	1913	1489	2537	2568	2845	3245	2659	1158	3
Radio	000 namba	103	56	72	102	108	95	54	76	
Betri	Millioni	24	35	21	44	47	53	57	58	

Chanzo Idara ya Takwimu

BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI ZA NJE(US$

MWAKA	1992	1993	1994	1995	1996
Mauzo	397.0	439.3	519.4	682.9	763
Manunuzi	1,316.6	1,274.9	1,309.3	1,340.5	1,212
Mauzo ya Bidhaa za viwandani nje	64.2	52.0	77.0	109.3	122
Mauzo ya Bidhaa zisizo za Asilia nje	165.50	183.10	182.52	299.37	327.
Mauzo ya Viwanda kama % ya mauzo nje	16	12	15	16	16
Mauzo ya Viwanda kama % ya Bidhaa zisizo Asilia	39	28	42	36	38
Mauzo nje kama % ya Manunuzi toka nje	30	34	40	51	63

Chanzo: Wizara ya Viwanda na Biashara